# KUSADIKIKA

*R. Mjema*

*Kusadikika* ni kitabu cha Shaaban Robert. Kitabu hiki kinahusu nchi ijulikanayo kwa jina la Kusadikika ni nchi iliyojiamini, "isiyokosea katika maamuzi yake" na "inayosadikiwa na watu wake".

**Uhusiano wa Kichwa na Maudhui**

(a) Habari zinazotolewa kitabuni zinahusu wakati katika nchi ya Kusadikika.
(b) Wajumbe ambao safari zao ndizo zilizotengeneza kitabu wanatumwa na nchi ya Kusadikika.
(c) Mhusika mkuu "Karama" ambaye tunamwona tangu mwanzo hadi mwisho anatoa utetezi wake katika baraza la Wasadikika. Hivyo basi tunaweza kusema upo muoano kati ya jina la kitabu na maudhui.

**Mtiririko**

Mwendo wa hadithi hii ni wa moja kwa moja. Sehemu ambayo tungeweza kidogo kuita kioo ni maelezo (mrejeo) au safari za wajumbe ambazo zilitokea zamani na msimulizi anaangalia nyuma.

(a) Hadithi inaanza na mashtaka yatolewayo na Waziri Majivuno. Anamshataki Karama kuwa ameanzisha shule ya Uanasheria ambao unapingana na sheria za Kusadikika.
(b) Baadaye Uanasheria unatafasiriwa na Karama baada ya kuruhusiwa. Yeye anasema kuwa "uaanasheria ni elimu ya hukumu kwa mujibu wa sheria zilizokubaliwa". Ndipo anapodhihirisha kuwa shule hiyo aliianzisha kwa sababu haikuwepo na akaendelea kuonyesha ukweli huo kwa kuwatumia wajumbe sita.
(c) Zinafuata safari za wajumbe na matokeo ya kila mjumbe.
(d) Kilele kinakuja wakati wa hukumu, pale mfalme alipoliruhusu baraza kutoa uamuzi. Uamuzi uliomtoa Karama hatiani na kuwafungua wajumbe wote.

**Lango**

***Kubeza***

Nia hasa ya mwandishi ni kutoa kitabu kinachobeua utawala wa wachache. Utawala ambao hautaki mapinduzi ya maamuzi na ya kifikira, usioruhusu mawazo ya wachochole wala maswali katika maamuzi. Nchi ambayo inaamini uwongo wa

kuificha haki. Majivuno anasema "Kusadikika imetukuka u1imwenguni kwa haki" (uk. wa 5). Shaaban anabeua utawala kwa kicheko cha uchungu, bila kusema waziwazi. Ndiyo kusema na mwandishi ametumia mtindo wa Ishara kutolea lango lake.

***Mapinduzi***

Anataka kuleta mapinduzi Serikalini na hasa kusawazisha makosa yatokeayo, hasa ya kisheria.

***Ujumbe.***

Anajaribu kutoa ukweli kuwa maishani binadamu hawezi kukaa na kukandamizwa siku zote, hata akiwa mwoga nia ya kutaka kuwa huru inamsukuma i1i kuitafuta haki yake. Siku moja mtu mmoja atajitokeza kwa niaba ya jamii kupigania haki, kama Karama.

***Utabiri***

Ametabiri mambo ambayo Tanzania tunayafuata siku hizi. Kufanya kazi kwa pamoja (Ujamaa), Uhuru, siasa isiyofungamana na upande wowote, umuhimu wa utamaduni, kufuta ubaguzi, kujenga umoja wa kimataifa bila kujali rangi, kilimo, vita n.k.

**Wahusika**

Wahusika katika "Kusadikika" ni bapa, hawaaminiki katika maisha. Mtunzi amefanya hivyo ili aonyeshe upande mmoja wa mawazo yake. Majina yao yanachukuana na kazi zao, pia tabia zao. Mfano:

| | | |
|---|---|---|
| Komeo | - | Huyu ni mlinda nchi, ni mtu asiyeruhusu mtu anayeleta mambo kinyume cha sheria (sadiki). |
| Majivuno | - | Anaaminika kuliko wote na ana akili na ni bora, kila analolisema ni la kweli au sawa. |
| | - | Anajisifu na muonevu, anajiamini kupindukia. |
| Mfalme | - | Ana busara kidogo, alimruhusu Karama ajitetee. |
| | - | Ana shauku ya elimu. Alionyesha nia ya elimu ya kutaka ajue maana ya Uanasheria. |
| Wasadiki | - | Walikandamizwa kiakili. |
| | - | Wanaipenda nchi yao, kwani walikubali kwa nia moja kujitolea kwa wajumbe sita. |
| Karama | - | Mwanamapinduzi, shujaa na mwenye busara. |

- Anajitoa nafsi yake kuleta haki na uhuru katika nchi yake.
- Amepewa vipawa vi tatu: ushujaa, ufasaha na hekima.

**Uhusiano na Maisha**

Nchi zote zilizopo au zilizokuwa chini ya utawla wa kigeni k.v. Zimbabwe, Guinea Bissau, Afrika ya Kusini n. k., tunaweza kuzifananisha na Kusadikika. Mtunzi ametaka kutuonyesha haya yafuatayo:

***Bidii ni ngazi ya mafanikio***

Bidii za Karama zimeiletea nchi yake faida ya kutambua kosa lake.

***Dhuluma***

Utumiaji mbaya wa vyeo. Majivuno ametumia cheo chake kuwanyanyasa watu wadogo wa Kusadikika.

***Haki ya mtu haipotei***

Haki ni kitu ambacho binadamu anaweza kukipoteza kwa muda tu lakini kwa njia moja au nyingine itamrudia. Karama, Wajumbe sita, na Wasadikika waliokuwa wakinyanyaswa, wakinyimwa uhuru na haki za kutoa mawazo yao mwisho wakazipata.

***Ubaya na Uzuri* wa *Sheria na Haki***

Sheria zinaweza zikawa chombo cha uonevu iwapo makusudi yake yatakuwa kwa manufaa ya wachache. Hivi ndivyo ilivyokuwa Kusadikika. Vilevile Sheria zinaweza kuwa chombo cha kuleta haki na ustawi nchini iwapo Sheria zitawekwa kwa faida ya watu wote, hii ndiyo haki aliyopigania Karama.

***Imani ya watu (Watawala)***

Kila kipya kilionekana ni kipingamizi, mawazo hayo Karama anasema yanatakiwa kuchunguzwa zaidi. Mtu hana budi kuchukua ya kale na ya sasa na kuyaweka kwenye mizani kabla ya kutoa uamuzi wowote. Kusadikika haikuwa na nafasi kama hiyo ya watu kama Majivuno. Penye nia, njia haikosekani. Mfano mzuri ni wa Karama.

**Maswali ya Kujadili**

"Kusadikika" ni kitabu cha mapinduzi. Jadili.

*Vidondoo*

Utawala ulishikwa na Majivuno.

(a) Ana uwezo wa kuvunja maisha ya mtu yeyote.
(b) Usemi wake haubadiliki "kipawa kisichokuwa na kiasi"
(c) Hakuna ruhusa ya kutoa mawazo au kufikiri.
(d) Hakuna swali lolote juu ya tendo lolote linaloamuliwa.
(e) Watawala walijiamini kupita kiasi. Watawaliwa walifikiriwa wajinga.

***Kupuuzwa***

(a) Uanasheria ni shughuli za watawala sio za Kabwela.
(b) Makabwela wote hawawezi kufikiri na kujiona watawala bora kuliko wengine.
(c) Waziri anasema "watu wa hali aliyonayo mshatikiwa, wafunzwe kuzielewa hali zao (uk. wa 3).
(d) Wasadikika walifanywa waumini wa utawala wa Majivuno.
(e) Usawa haukuwepo, watoto wa matajiri ndio walofaidi katika nchi.

***Uonevu***

(a) Maisha ya watu hayakujaliwa, ukulima, ufugaji n.k
(b) Ushirikiano katika kazi haukuwepo.

***Mapinduzi kwa Vipi?***

(a) Karama anachukua nafasi ya uzalendo hasa. Amejitokeza katika nchi isiyo na huruma tayari kwa lolote. Ni mkombozi wa wajumbe sita na nchi nzima. Amefungua mlango ili Kusadikika ipate kutumia akili.
(b) Ushindi wa Karama unatoa ubaya wa utawala usio na haki na unabomoa kuta kwa kuwatoa wajumbe.
(c) Watu wanapata uhuru. Haya ni mapinduzi makubwa ya Kusadikika.
(d) Ameleta mapinduzi ya kisiasa; mawazo yanaingia.
(e) Kiuchumi - ukulima unabadilika na maisha kwa jumla.

MAKTABA
TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI

*Wajumbe*

Hao pia walitaka mapinduzi, walijitolea ili kuimarisha nchi, walikuwa tayari kufia haki.

**Maswali ya Kujadili**

1. Kwa nini Shaaban Robert ameandika kitabu cha Kusadikika katika mtindo wa Fumbo na hata kusema kuwa nchi ya Kusadikika ipo ndotoni tu?
2. Nchi ya Kusadikika ilikuwa nchi ya namna gani?
3. "Tunasema kuwa nchi ya Kusadikika ni mfano dhahiri wa nchi zilipo au zilizokuwa chini ya utawala wa kikoloni." Pinga au unga mkono usemi huo kwa mifano dhahiri ya nchi uzifahamuzo katika Afrika.
4. "Karama amejitokeza kama mwanamapinduzi halisi". 'Jadili usemi huo.
5. "Nitakuwa tayari kujitolea nafsi yangu kwa faida ya nchi yangu na raia wake."Je usemi huo unakubalika katika kitabu cha Kusadikika? Toa maelezo na mifano toka hadithini inayokanusha au kuukubali usemi huo.
6. "Hekima ni kitu adimu kupatikana kwa watu wasio mvi."
   (a) Nini maana ya usemi huo? Kwa nini umetamkwa?
   (b) Andika usemi mwingine toka kitabuni unaokanusha huo hapojuu.

**Lugha**

***Mafumbo:***

Hadithi yote imewekwa katika lugha ya mafumbo

Anasema

- Ng'ornbe akivunjika...."

-Anaficha siri kama kaburi-

***Kejeli***

Anamkejeli Waziri

"...sababu ya tabia yangu njema"-

"Wafalme na raia.... ni watu wasiosema uongo"

***Fasili* ya *Binadamu***

Dharau itafunua kinywa ....iteme mate kama bafe..."

-jinsi itatoka irande...."

***Hana Lugha ya Kashfa***

Jibu la kukanusha kipimo cha elimu na mvi.

***Kebehi (mshangao)***

Miisho yote ya kila sura ya wajumbe wake.
"Moyo wa nani usohuzunika kwa msiba kama huo."

***Muundo***

(i) Kitabu kimegaiwa katika sura tisa. Hadithi hii ni ya kubuni, pia ni fumbo alilotoa Shaaban. Ni hadithi ya moja kwa moja.

(ii) Kila sura katika utetezi ameimaliza kwa swali la mshangao na kebehi.

***Mfano***

"Macho ya nani yasiyolengwalengwa machozi kama huo". Karama amechukua nafasi ya mwandishi, hivyo mtunzi anaongea kupitia kwa mhusika wake mkuu (Karama). Msimamo wa Karama ndiyo wa mtunzi mwenyewe.

***Wahusika***

Wahusika wake wako bapa. Hawaaminiki kimaisha. Amewagawa katika makundi mawili, wabaya na wema. Kila jina limebeba tafsiri ya tabia yake. Kuna wahusika wakuu na vikaragosi. Mfano: Mudri wa sheria na Mfalme, wanaonekana mwanzo na mwisho. Hatuwaoni wakiongea sana.

**Kufaulu: Sanaa na Maudhui**

Kutokana na maana ya kitabu chenyewe mtunzi amefaulu.

1. Ametoka kwenye uandishi wa kila siku na kuwaingiza wasomaji kwenye Ishara.
2. Wahusika wake kuwa bapa si kitu cha kawaida ila ni mtindo mpya tofauti na mitindo ya watunzi wengi.
3. Ameweza kucheza na sanaa kuanishia mawazo yake na mazingira.
4. Miisho ya sura ya utetezi wake ina msisimuo na mchomo ambao kwanza unamfanya msomaji na hasa muamuzi kumhurumia mhusika.
5. Amelieleza vižuri sana suala 1a ukoloni, ukombozi na siasa safi ya kufuatwa.

(Makala haya yalitolewa kwa mara ya kwanza katika jarida la MULIKA Na. 12, Machi, 1978) .